



## ***Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo***

### **1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01- 10 APRIL, 2024 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 11- 20 APRIL, 2024**

#### **1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 01- 10 APRIL, 2024**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene iliimarika kidogo wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilidhohofika kidogo. Hali hii ilisababisha ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kubakia katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu. Joto la bahari katika eneo kubwa la magharibi mwa Bahari ya Hindi lilikuwa la juu ya wastani ukilinganisha na eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi, hali hii ilisababisha kuvuma kwa upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua.

#### **1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01- 10 APRIL, 2024**

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria, magharibi, kusini, nyanda za juu kusini-magharibi, maeneo ya nyanda za juu kaskazini-mashariki na katika maeneo ya ukanda wa Pwani. Maeneo ya ukanda wa kati yalipata mvua nyepesi hadi za wastani.

### **2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11- 20 APRIL, 2024**

#### **2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 11- 20 APRIL, 2024**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika kidogo wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kudhohofika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kuwepo katika maeneo ya kaskazini mwa nchi yetu. Joto la bahari katika eneo kubwa la magharibi mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu ya wastani ukilinganisha na eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi, hali hii inatarajiwa kusababisha kuvuma kwa upepo wenye

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)

unyevunyevu ktoka baharini kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua.

## **2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 11- 20 APRIL, 2024**

**Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo mengi.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Vipindi vya ukavu kwa ujumla vinatarajiwa.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Imetolewa na;

## **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)